

102/2

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA MTHANI

### UFAHAMU

- a) Kutenda haki/sharti tutende haki  $1 \times 1 = 1$
- b) (i) Unachangia kuvumilia bila kusuta wengine  
(ii) Tunajifunza juu ya sheria na haki za watu  $(2 \times 1 = 2)$
- c) (i) kutopiga yowe dhidi ya ubakaji  
(ii) Kutopiga yowe mume anapompiga mwanamke hadi kifo  
(iii) Kutopiga yowe dhidi ya wizi wa mabavu  $(3 \times 1 = 3)$
- d) (i) Inaegemea wananchi wasioangazia amani  
(ii) Walinda usalama  $(2 \times 2 = 4)$
- e) (i) Haijalishi ni nani anayehusika kwani sheria inapaswa kufuatwa kwa wote bila kubagua awe mkubwa au mdogo, kiongozi wa dini au mtu wa kawaida  
(ii) Ukweli ni lazima usemwe kuondoa wasiwasi uliopo kati ya watu  $(2 \times 1 = 2)$
- f) (i) Kuwafikisha kortini na haki kutendeka  
(ii) kutokuwa na mapendeleo  
(iii) Kupewa adhabu kali/inayofaa  $(2 \times 1 = 2)$
- g) (i) Uradidi- “yapo ya”imerudiwa  
(ii) chuku- mashabiki kufanya timu ishinde kombe la dunia  
(iii) balagha- mbona hatupigi yowe dhidi ya ubakaji  $(2 \times 1 = 2)$


### MATUMIZI YA LUGHA

- (a) Mwalimu anamsahihishia Kamene zoezi  $(1 \times 2 = 2)$
- (b) (i) Mkao wa midomo  
(ii) Mahali katika ulimi  
(iii) Ulimi huwa wapi kinywani  $(3 \times 1 = 3)$
- (c) Ni mofimu ambayo hujisimamia na kuwa na maana kamilifu. Mfano baba, mama, sana, mno n.k. (Maana alama I Mfano alama 1)
- (d) Sauti, silabi, neno na sentensi  $(\frac{1}{2} \times 4 = 2)$
- (e) (i) Ni tungo la kisarufi lenye muundo wa kiima na kiarifa na hupatika katika sentensi  $(1 \times 1 = 1)$   
(ii) Kitabu kilichonunuliwa dukani ni changu **au** Ng’ombe ambaye anaugua atatibiwa leo  $(1 \times 2 = 2)$
- (f) Mvule alikuwa bwenini  $(1 \times 2 = 2)$
- (g) **Nanyi**- ufupisho wa nafsi  
Nendeni- kuonyesha wingi

**Kinyama** – kuunda kielezi cha namna mfanano

**Kwa** – kuonyesha sababu ( $\frac{1}{2} \times 4 = 2$ )

- (h) Teo lililonunuliwa limezeeka ( $\frac{1}{2} \times 4 = 2$ )
- (i) Unaweza kwenda uwanjani sasa *madhali* umekamilisha kazi yako ( $1 \times 2 = 2$ )
- (j) (i) jiwa  
(ii) chika ( $2 \times 1 = 2$ )
- (k) Baba aliwanunua ng'ombe wawili mwaka '10 ( $2 \times 1 = 2$ )
- (l) Ukilipa uingie ndani ( $2 \times 1 = 2$ )
- (m) LI- YA ( $1 \times 1 = 1$ )
- (n) “Hirshi, nakuomba uje hapa nilipo ili nikutume,” Kassim alisema. ( $1 \times 2 = 2$ )



### ISIMUJAMII (Alama 10)

#### Sifa za sajili ya siasa

- (a) Matumizi ya msamiati wa kisiasa kama vile uchaguzi, kura, mbunge, sheria n.k
- (b) Msamiati wa heshima- Nawaomba wananchi watukufu mnipigie kura
- (c) Matumizi ya lugha iliyojaa hadi mfano, mkinichagua nitawajengea hospitali, shule zaidi na kuwapa kazi vijana wote
- (d) Wanasiasa wengine huharibu lugha katika uteuzi wao wa msamiati. Mfano hii uchaguzi mpaka mtu aangushwe
- (e) Kurudiwarudiwa kwa kauli kama njia ya kusisitiza jambo lisemwalo. Mfano, Mimi nimeleta maendeleo, nikaleta maji, nikaleta stima, nikaleta sipitali...mwataka nani mwingine kweli?
- (f) Mazungumzo huendelezwa kwa nafsi ya kwanza. Mfano, Mimi nimewatetea bungeni, nikaungana nanyi hapa, tukashikana mikono mpaka tukapata haki yetu
- (g) Matumizi ya maswali ya balagha mfano, Msiponipa kura zenu, nani mwingine?

- (h) Kuna matumizi ya mbinu ya tawasifu mfano, Mimi ndiye kiongozi aliyezindua mradi huo, nikamwalika kiongozi wa kitaifa akaja kuufungua kwa sababu anaheshimu kazi yangu nzuri (5x2=10)